



Tafsiri na Ukalimani Barani Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara: Changamoto Mpya katika Ulimwengu wa ulumbi

Mwito wa Makala kwa Uchapishaji wa Kitabu kwa pamoja

Wahariri: Justine Ndongo-Keller, Évariste Ntakirutimana,
Mame Thierno Cisse na Marc Van Campenhoudt

Mnamo Februari, katika Chuo Kikuu cha Cheikh Anta Diop, mjini Dakar, Mtandao wa Leksikolojia, Istilahi na Tafsiri (LTT) uliandaa kongamano lenye mada ya "Kuelezea turathi za kiisimu na kitamaduni katika huduma za ulumbi Barani Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara". Kutokana na mkutano huo, Mtandao wa LTT, ukisaidiwa na Chama cha Vyuo Vikuu vinavyotumia lugha ya Kifaransa, uliandaa semina iliyokuwa ikimakinikia uendelezaji wa mitaala ya lugha za Kiafrika zinazolenga watafsiri na wakalimani wa Kifaransa, ikisukumwa na haja ya kujaribu kutaalamisha ufundishaji wa lugha na sanaa.

Mitaala kama hiyo tayari inapatikana katika mataifa ya Afrika ya Kaskazini. Mnamo 2009, Ofisi ya Umoja wa Mataifa jijini Nairobi ilizindua Ushirikiano wa Kipanafrika katika Shahada ya Uzamili kuhusu Ukalimani na Utafsiri (PAMCIT), ambao unaleta pamoja vyuo vikuu sita: Chuo Kikuu cha Nairobi, nchini Kenya, Chuo Kikuu cha Legon nchini Ghana, Chuo Kikuu cha Buea (ASTI) nchini Cameroon, Chuo Kikuu cha Maputo, nchini Msumbiji, Chuo Kikuu cha Gaston Berger de Saint-Louis, nchini Senegal na Chuo Kikuu cha Cairo, nchini Misri. Programu nyingine za uzamili zinaendelea kuandaliwa pole pole, kama ilivyo nchini Rwanda, kwa ufadhili wa Mtandao wa LTT na Chama cha Vyuo vikuu vinavyotumia lugha ya Kifaransa, huku shule za vyuo vikuu zilizoimarika zikijaribu kujizindua upya, mara nyingine kwa msaada wa mashirika ya kimataifa.

Mashirika makuu ya kimataifa katika bara la Afrika yanaendesha idara za tafsiri na ukalimani (kwa mfano Umoja wa Mataifa jijini Nairobi, Umoja wa Afrika jijini Addis Ababa, na kadhalika). Hata hivyo, zaidi ya mifumo ya kimapokeo ya ukalimani na tafsiri kwa mahitaji ya uhusiano wa kimataifa yanayotumia lugha za kikoloni kimsingi, kuna haja kubwa ya kuwekeza katika ukalimani na tafsiri kwa huduma za umma katika lugha za kitaifa za raia wa nchi za Kiafrika, ambao wanatambua uanuwai wa kilugha na changamoto za kimawasiliano ambazo zimeibuka kutokana na lugha rasmi zilizorithiwa kutoka ukoloni na kuruhusu lugha hizi za kitaifa katika mabunge ya kidemokrasia au kupanga hata ukalimani sambamba (tukiwazia mabunge ya Afrika Kusini, Kenya, Tanzania na Senegal na pia Bunge la Afrika). Kwa ujumla, jambo muhimu kwa Serikali sasa, ni kuwafundisha wataalamu wa lugha wa kutegemeka katika ukalimani na tafasiri mashinani. Mashirika mengi yasiyo ya kiserikali, wataalamu wa nchini na wa kimataifa na

wanahabari, daima wanakumbwa na changamoto za kuwasiliana na umma ulio mashinani bila hata wao kutambua kuwa tatizo hilo lipo. Kuna haja ya “ukalimani wa kijamii” ambao unahusisha hospitali, wilaya, mahakama, huduma za kijamii, mashirika, kambi za wakimbizi, na kadhalika. Maendeleo ya haki za kimataifa yameibua suala muhimu la ukalimani wa mahakama na haja isiyoweza kukidhiwa ya uelewano wa pamoja baina ya lugha za kiulaya na lugha za mashahidi, wahanga au wanaojitetea (kwa mfano lugha ya Kinyarwanda katika Mahakama ya Kimataifa ya Jinai ya Rwanda, lugha ya Krio katika Mahakama Maalum ya Sierra Leone, na lugha ya Sango katika Mahakama ya Kimataifa ya Jinai).

Pakiwa na visa vingi vya upelelezi, ripoti na miradi, masuala yanayohusiana na elimu yanaonekana kuwa muhimu sana katika bara ambalo lina sifa za utajiri wa uanuwai wa kilugha. Katika mazingira haya, bila shaka kuna swali la elimu iliyo na msingi wake katika nguvu zisizoepukika za ulumbi katika mataifa ya Kiafrika: je, matumizi ya pamoja ya lugha za Kiafrika na lugha za kiulaya ndani ya mfumo wa mtazamo uliojengeka (kwa mfano mradi wa ELAN-Africa (Unaohusu Mfumo wa Kitaifa wa Masomo na Lugha- ambao ni mradi wa kuinua elimu ya ulumbi katika Mataifa ya yanayotumia Kifaransa), Mifumo ya Elimu iliyoshirikisha Maarifa na Lugha (CLIL)) yanaweza kukabiliana na baadhi ya vikwazo vya maendeleo? Hili huhitaji, kama katika kila kazi ya tafsiri na ukalimani, vifaa vya kisasa, utengenezaji wa vielelezo vya lugha fulani na utungaji wa istilahi mpya zinazolingana na mahitaji. Uwezeshaji wa lugha za kiasili utahusisha tafsiri za kazi muhimu na maarufu katika nyanja za kisayansi, kifasihi na kifalsafa...na uhamasishaji wa maandishi kwa lugha za bara hili. Ujenzi wa kongoo kubwa (iliyooanishwa na kuhifadhiwa kikompyuta) kunaweza kuchangia pakubwa katika malengo haya, kupitia uundaji wa kamusi. Hata hivyo, haya yote tuliyotaja hayawezi kushughulikiwa kikamilifu bila kuhusisha utafiti na uchunguzi ambao tayari umefanywa kwa miaka mingi na unahitaji kukumbukwa na kushirikishwa.

Mtandao wa LTT unazindua mwito wa makala kwa uchapishaji wa pamoja wa kitabu ambacho sura zake mbali mbali zinayazungumzia masuala yote haya. Michango hii itahusu tajriba, maelezo ya masuala, ufafanuzi wa mbinu za utafiti, ukaguzi, uchunguzi wa kijuujuu na kadhalika. Makala yanapaswa kufuata kanuni za uhariri na kuwasilishwa kufikia tarehe 1 Julai 2017 kwa barua pepe contact@reseau-ltt.net. Makala hizo zitaandikwa kwa lugha rasmi za Muungano wa nchi za kiafrika, na kuwa na urefu usiozidi maneno 40,000 (bila nafasi), yakiwemo marejeo na viambatisho vya ziada.

Mradi wa uchapishaji utaongozwa na wataalamu wakishirikiana na kamati ya kisayansi iliyoundwa kwa ajili hiyo wengi wakiwa wanatoka kwenye maaraba wanachama wa Mtandao wa LTT na wataalamu wengine kulingana na mahitaji ya kilugha. Katika mapitio ya kisayansi, kila makala itapitiwa na wataalamu wawili wa kamati hiyo, akiwemo mmoja kutoka bara la Afrika. Kukitokea maoni tofauti, utathmini wa tatu utahitajika. Ili kufanikiwa kuchapishwa, nakala ya mwisho ya makala sharti iwe inafuata maoni yaliyotolewa na wataalamu.

Kalenda iliyopendekezwa

- 1 Aprili, 2017 : Kutangazwa kwa mwito wa makala
- 1 Julai, 2017 : Mwisho wa kupokea makala
- 1 Novemba, 2017 : Maoni ya Kamati ya Kisayansi
- 1 Januari, 2018: Mwisho wa kupokea nakala safi ya makala
- 1 Aprili, 2018 : Uchapishaji wa KitabuIn February 2014

Kamati ya wataalam

Ibrahim Ben Mrad (Université de Tunis La Manouba)

Xavier Blanco Escoda (Universitat Autònoma de Barcelona)

Mame Thierno Cisse (Université Cheikh Anta Diop de Dakar)

Manuel Celio Conceição (Universidade do Algarve)

Marcel Diki-Kidiri (African Academy of Languages and Maaya Network)

Abubakar Katerrega (University of Rwanda)

Noël Muylle (DG Interpretation)

Piet Van de Craen (Vrije Universiteit Brussel)

Gabrielle Le Tallec Lloret (Université de Paris 13)

Xavier Luffin (Université libre de Bruxelles)

Justine Ndong-Keller (University of Nairobi)

Laurent Nkusi (University of Kibungo)

Évariste Ntakirutimana (University of Rwanda)

Marc Van Campenhoudt (Université libre de Bruxelles)
